JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS -TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA.

+255755439313 –Mkuu wa Shule
+255759044738 –Makamu wa Shule
+255769621477- Mwl Taaluma
+255767908238–Mwl Mlezi
+255758983440- Mwl wa darasa

S/Sekondari Malampaka,

S.L.P.82,

MASWA.

29/03/2022

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI _____

S.L.P _____

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MALAMPAKA, HALMASHAURI YA MASWA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2022.

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2022 tahasusi ya .....
Shule ya Sekondari **MALAMPAKA** ipo umbali wa Kilometa 02 Mashariki mwa mji wa MALAMPAKA. Usafiri wa basi kutoka mjini MWANZA/SHINYANGA/MASWA unapatikana katika kituo cha mabasi NYEGEZI/SHINYANGA/MASWA. Nauli ya kufika shuleni ni kati ya shilingi 3000-6000, kutegemea unakotokea. Aidha kuna usafiri wa gari moshi (treni) toka Dar es salaam, Dodoma,Tabora na Mwanza, kituo cha kuteremkia ni Malampaka kisha unachukua usafiri wa pikipiki mpaka shuleni.

Muhula wa masomo unaanza tarehe ..... Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..... isipokuwa kama itatangazwa vinginevyo. Mwisho wa kuriport ni wiki mbili au siku 14 tu baada ya kutangazwa muda wa kuripoti.

***Tarehe ya kufungua shule itatangazwa na Wizara**

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:**
   2.1. Sare ya shule
   a) Sare ya shule hii ni suruali 2 nyeusi rinda 2 na mfuko 1 nyuma chini ukubwa 16 inch, mashati meupe 2 mikono mirefu.
   b) Sare ya michezo ni Tracksuit 1 rangi ya bluu na viatu vya raba vyeusi.
   c) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
   d) Soksi jozi mbili nyeusi za shule.
   e) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.
   f) Sweta rangi ya bluu yenye mikono mirefu aipate dukani kabla ya kufika shuleni.
   g) Nguo za kushindia (after classes dress) suruali 2 ya kaki rinda 2 na mfuko 1 nyuma chini ukubwa 16 inch.
   h) Tai 2 zenye rangi ya suruali ya shule.
   i) T-Shirt 2 rangi kijivu yenye collar nyeusi, nembo na maandishi ya Shule - aipate dukani atakapoelekezwa .(maelekezo ya upatikanaji wa T-shirt yatatolewa shuleni)
   (kofia na nguo za nyumbani haziruhusiwi)

Angalizo. Picha ya sare na namna ya uvaaji wa mwanafunzi imeambatanishwa.

2.2. **Ada na michango ya shule.**

a) Ada ya shule kwa mwaka ni Tshs **70,000**. Unaweza kulipa kiasi cha Tshs **35,000** kwa muhula au kulipia ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **BENKI YA NMB ACCOUNT NUMBER 30801100097 JINA LA ACCOUNT NI "MALAMPAKA SEKONDARI (TAFADHALI ANDIKA JINA LA MWANAFUNZI KWENYE PAY SLIP)**. Mchanganuo wa michango hiyo ni kama ifuatavyo:-

ADA	70,000.00	KWA MWAKA
TAALUMA	20,000.00	KWA MWAKA
WALINZI NA WAPISHI	30,000.00	KWA MWAKA
UKARABATI	15,000.00	KWA MWAKA
TAHADHARI	5,000.00	HAIRUDISHWI
MITIHANI YA KUJIPIMA (MOCK)	20,000.00	
HUDUMA YA AFYA	10,000.00	
KITAMBULISHO NA PICHA	6,000.00	
NEMBO	2,000.00	
JUMLA YA MICHANGO YOTE	**178,000.00**	**KWA MWAKA**

b) Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kujanayo shuleni ni:

i. Ream 2 ya karatasi (kwa mwaka).
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa).
iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa biolojia.
iv. Scientific calculator CBG na PCB tu.
v. Godoro la inch 2.5 x 6
vi. Mashuka pair 2 rangi ya bluu, blanket 1, foronya 1 rangi ya bluu na chandarua
vii. Vyombo vya kulia chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).
viii. Ndoo mbili za plastiki zenye mifuniko.
ix. Jembe na mpini 1, Reki na mpini 1, mfagio wa ndani 1 na nje 1, squizer/mopa na fyekeo 1
x. Galoni ya lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa
xi. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
xii. Result slip.
xiii. File moja ya kutunzia kumbukumbu.
xiv. Oxford dictionary(current Edition)

Angalizo: vifaa vyote vitakaguliwa mwanafunzi anaporipoti shuleni

3. WAJIBU WA MWANAFUNZI

i. Kuamka asubuhi na mapema na kuitikia wito kwa haraka kila unapohitajika.
ii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
iii. Kuvaa sare ya shule wakati wote uwapo shuleni, nje ya eneo la shule na safarini.
iv. Kuhudhuria masomo siku zote za masomo
v. Kuepuka utoro, uzembe,udanganyifu na uhuni wa kila aina.
vi. Kuwa na nidhamu ya hali ya juu mahali popote.
vii. Kushiriki kikamilifu katika kazi za shule michezo na utamaduni.
viii. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo shuleni wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
ix. Kushiriki katika shughuli zote zinazokujenga kuwa raia mwema.
x. Mwanafunzi sharti aonekane nadhifu wakati wote.

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kupaka kucha rangi, kupakaa rangi mdomoni, kutunza kucha ndefu, kutinda nyusi na kupaka wanja wakati wote ukiwa shuleni.

xii. Unatakiwa kuzingatia wajibu wako kama mwanafunzi. Unatakiwa kudumisha amani, nidhamu, ushirikiano, utendaji kazi kwa heshima na kwa kila mtu, wanafunzi wenzako, walimu, wafanyakazi wasio walimu, wanakijiji na viongozi wote. Unatakiwa kusalimia wakubwa wako.

4. MAWASILIANO NA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI.

Mwanafunzi atakapokua shule atakua chini ya usimamizi wa walezi wa darasa na bweni. Utawasiliana na mlezi wa darasa au bweni husika kwa masuala mbalimbali hasa huduma ya kifedha kwa mwanao, Mwanafunzi atakapofika shuleni atajulishwa bweni lake.

Mawasiliano kati ya mzazi na shule ni ya mkuu wa shule, aidha mwanafunzi anaweza kutumia simu silizo orodheshwa hapo juu kuwasiliana na mzazi. **EPUKA MATAPELI.**

S/NO	JINA LA BWENI	JINA LA MWALIMU MLEZI	NAMBA YA SIMU
1	SERENGETI	SALVATORY ANGELO	0762459118
2	NGORONGORO	FABIAN MBUBILANYA JILES	0622144871
3	MIKUMI	CHARLES SANKA STEPHANO	0621040983

5. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

a) Kila mwanafunzi anatakiwa kutumia busara (common sense) katika maisha yote awapo shule.
b) Wanafunzi lazima wawe na heshima na utu kwa watu wazima na kati yao wenyewe.
c) Ni wajibu wa mwanafunzi kutunza na kuangalia mali ya shule na yake binafsi.
d) Wanafunzi hawaruhusiwi kufika nyumbani kwa walimu bila ruhusa ya patroni.
e) Ni marufuku kuingia katika nyumba za starehe kama vile Baa, dansi na nyumba za kulala wageni (Guest house).
f) Ni wajibu wa mwanafunzi kutunza mazingira ya shule , madarasa, vyoo na vyumba vingine shuleni katika hali ya usafi.
g) Matusi ya kusema au kuandika na ugomvi ni marufuku shuleni
h) Mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi kwa masomo yote. Aidha ni lazima kuhudhuria vipindi vya dini yake kila siku kadri ya ratiba iliyopangwa.
i) Ni mwiko kwa mwanafunzi kujiunga na vikundi nyenye tabia mbaya popote pale ndani na nje ya shule.
j) Kila mwanafunzi anapaswa kuwahi shuleni kwa muda ulopangwa.
k) Ni marufuku kupokea wageni wa kwako binafsi uwapo shuleni.(Aidha siku ya kutembelewa shuleni ni jumapili ya mwisho wa mwezi)
l) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa.
m) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga kelele awapo darasani.
n) Mwanafunzi atunze nywele zake zikiwa fupi. Ni marufuku kuweka dawa (curl au relaxer) kwenye nywele.
o) Ni marufuku mwanafunzi kufuga kucha ndefu na kuwa na nywele ndefu. Mwanafunzi haruhusiwi kunyoa kipara, panki, kiduku na kutinda nyusi za macho / usoni.
p) Mwanafunzi anapaswa avae sare wakati wote awapo shule na nje ya shule.
q) Urafiki wa mwanafunzi wa kike na kiume uwe ule wa kaka na dada.

6. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
vi. Kufuga ndevu.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya au Uvutaji wa sigara.
viii. Uasherati, kuoa au kuolewa.
ix. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
x. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana au kushawishi kutoa mimba.
xi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xii. Kumiliki,,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiii. Kudharau Bendera ya Taifa.
xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xv. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xvi. Kosa lolote kubwa ambalo uongozi wa shule utaamua mwanafunzi anastahili adhabu kama hiyo.

7. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya Serikali.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi.
c) Mkataba wa kutoshiriki katika mgomo,fujo na makosa ya jinai.
d) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
e) Picha nne passpot (4) za Wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kutekeleza kikamilifu.Aidha mzazi mpe mwanao nauli ya kurudi nyumbani kwani anaweza kurudishwa nyumbani muda wowote pindi akishindwa kufata na kutii sheria za shule.

KARIBU SANA MALAMPAKA SEKONDARI.

.....

MALOSHA M. PAULINE

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MALAMPAKA
S.L.P. 82 MALAMPAKA
MASWA

MASWA DISTRICT COUNCIL

MEDICAL EXAMINATION REQUEST FORM

To be filled by an Authorized Government Medical Officer and returned to School.

From: Malampaka Secondary School,
P.O.BOX 82,
MASWA.

To: THE MEDICAL OFFICER, ...

Ref: ..... (a student).

Please examine the above named student to ascertain his physical and mental fitness for a fulltime schooling course at this school .The examination should include categories I- IV.

Category I.

a) Eye sight:.....
b) Hearing:.....
c) Limbs:.....
d) Speech:.....
e) Venereal diseases:.....
f) Sickle cell anemia:.....
g) Tuberculosis (TB):.....
h) Asthma:.....
i) Heart problem:.....
j) Kidney:.....
k) Peptic ulcers:.....
l) Epilepsy:.....
m) Leprosy:.....

Category II. Neurosis..... .....

Category III. Other Serious Diseases: .....

I (Full name).....have examined the above named and consider that he is Physically fit /unfit for a full time schooling course .

Designation..... Signature.....

Date: ...../ ...../..... Rubber stamp.....

TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

Sehemu hii ijazwe kwa kushirikiana na Mzazi / Mlezi

i. Jina kamili la mwanafunzi.....

ii. Tarehe ya kuzaliwa ..... mwezi..... Mwaka.....

iii. Uraia..... Kabila.....

iv. Dini yako..... Dhehebu lako.....

v. (a) Jina ka Mzazi/ Mlezi ..... hai / siyo hai

(b) Kazi ya Mzazi / Mlezi.....

(c) Mzazi / Mlezi anaishi ..... kata.....

(d) Anuani ya posta ya Mzazi/ Mlezi.....

(e) Namba ya simu ya mkononi ya Mzazi /Mlezi.....

vi. Taja tatizo la kiafya/ maumbile ulilonalo (onyesha cheti kama kipo)

.....

.....

.....

.....

.....

TAMKO LA MZAZI / MLEZI

Mimi..... (Jina Kamili) ambaye ni Mzazi /

Mlezi wa mwanafunzi huyu, ninakiri kuwa taarifa zake zilizoandikwa hapo juu ni sahihi. Aidha nakubali mtoto wangu asajiliwe katika shule ya sekondari Malampaka. Naahidi kutoa ushirikiano wa karibu katika kumlea na kumuendeleza kielimu. Pia ninakubali kumuwezesha kikamilifu kwa kumpatia mahitaji yake muhimu ya shule ili aweze kutulia shuleni na kuweka bidii katika masomo yake.

Saini..... .....

Tarehe .....

Namba za simu.....

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA
SHULE YA SEKONDARI MALAMPAKA
S.L.P 82 MALAMPAKA, MASWA

MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi .....wa Mtaa/kijiji cha .....

Kitongoji cha.....kata ya .....

Wilaya ya ..... amaye ni mhitimu wa Elimu ya kidato cha nne toka shule ya sekondari .....Naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ambao ni;

a) Jina .....Uhusiano.....

b) Jina .....Uhusiano.....

Kuwa kwa kipindi chote cha mwaka/miaka ..... ninachotarajia kuwepo Shule ya Sekondari Malampaka nikiwa kama mwanafunzi kwa namna yeyote ile sitoanzisha wala kushiriki katika migomo, fujo na kujihusisha katika makosa ya jinai kwa kisingizio chochote kile; kwani natambua kuwa matendo hayo husababisha hasara kubwa kwa Taifa. Hivyo nitakuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa kunakuwepo na amani na utulivu na pale nitakapoona haki haitendeki nitatumia taratibu zilizowekwa ili haki itendeke na si vinginevyo.

Endepo nitakiuka ahadi hii, natambua nimetenda kosa na ninastahili **KUFUKUZWA SHULE** kwa nitakuwa nimetenda kwa makusudi

Jina la Mwanafunzi.....saini.....

1. Jina la mzazi .....saini.....simu.....
2. Jina la mzazi .....saini.....simu.....
3. Jina la Mwenyekiti wa Mtaa..... saini.....simu.....

Tarehe..... Mhuri.....

SAINIYA MKUU WA SHULE .....TAREHE.....MHURI.....

ORODHA YA VITABU

1. HISTORY

1. ADVANCED LEARNER'S HISTORY 5 & 6 - OXFORD
2. MASTERING HISTORY CARTER - CARTER
3. HISTORY FOR ADVANCED LEVEL - ZISTI KAMILI
4. CONTEMPORARY HISTORICAL EVENTS, HISTORY ONE-COMRADE SHIBITALI CK
5. CONTEMPORARY HISTORICAL EVENTS, HISTORY TWO-COMRADE SHIBITALI CK
6. HISTORY ONE REVISION BOOK-COMRADE SHIBITALI CK
7. HISTORY TWO REVISION BOOK- COMRADE SHIBITALI CK

2. GEOGRAPHY

1. PHYSICAL GEOGRAPHY - MSABILA
2. HUMAN ECONOMIC GEOGRAPHY - MSABILA
3. PHYSICAL GEOGRAPHY - MONK HOUSE
4. PHYSICAL GEOGRAPHY - BUNNET
5. INTERGRATED GEOGRAPHY - DAVID WAUGH

3. ENGLISH LANGUAGE

1. ADVANCED ENGLISH LANGUAGE - OXFORD
2. ENGLISH LANGUAGE - NICHOLAUS ASHEL
3. ADVANCED LITERATURE - NICHOLAUS ASHEL
4. OXFORD ADVANCED DICTIONARY
5. ENGLISH LITERATURE BOOKS
   - ✓ Encounters from Africa
   - ✓ Rwanda Magere
   - ✓ His Excellence the Head of States
   - ✓ I will marry when I want
   - ✓ Betrayal in city
   - ✓ Devine Province
   - ✓ A man of the people
   - ✓ The Beautyful Ones are not yet born
   - ✓ The Bride
   - ✓ Black Mamba
   - ✓ Selected poem

4. BIOLOGY

- BIOLOGICAL SCIENCE FOR ADVANCED LEVEL 02nd or 03rd Edition
- UNDERSTANDING BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL

5. CHEMISTRY

- CONCEPTUAL CHEMISTRY - CHAND VOL. XI, XII
- RAMSDEN - 04TH Edition

6. PHYSICS

- PRINCIPLES OF PHYSICS FOR CLASS XI (S. CHAND'S)
- PRINCIPLES OF PHYSICS FOR CLASS XII (S. CHAND'S)
- ADVANCED LEVEL PHYSICS 7TH EDITION (MICHAEL NELKON)
- ADVANCED PHYSICS (LOGER MANKASTER)

7. ADVANCED MATHEMATICS

1. PURE MATHEMATICS 1 & 2 - AUTHOR BACKHOUSE
2. ADVANCED LEVEL MATHEMATICS - C.J TRANTER
3. ADVANCED LEVEL MATHEMATICS - CHAND
4. ENGINEERING MATHEMATICS -
5. CONSCISE MATHEMATICS - BOSTOCK & CHANDLER

8.KISWAHILI

1.NADHARIA YA LUGHA KIDATO CHA TANO NA SITA-J.A MASEBO
2. KAMUSI YA KISWAHILI
3.NADHARIA YA LUGHA - C. M SALUHAYA
4.NADHARIA YA FASIHI -J.A MASEBO
5. RIWAYA;
   - ✓ KUFIKIRIKA-SHABAN ROBERT
   - ✓ USIKU UTAKAPOKWISHA-M. MSOKILE
   - ✓ VUTA n'KUVUTE-S.A .SHAFI
   - ✓ MFADHILI H. TUWA
6. USHAIRI;
   - ✓ FUNGATE YA UHURU
   - ✓ KIMBUNGA
   - ✓ MAPENZI BORA
   - ✓ CHUNGU TAMU

   TAMTHILIYA
   - ✓ NGUZO MAMA
   - ✓ KWENYE UKINGO WA THIM
   - ✓ MORANI
   - ✓ KIVULI KINAISHI

Kielelezo cha sare za kuvalia darasani



Kielelezo cha sare za kuvalia baada ya vipindi vya darasani na wakati wa michezo